# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA TANO

**14 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA TANO – TAREHE 14 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**55. MHESHIMIWA AZIZA SLEYUM ALLY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Maboma ya Zahanati na Shule yaliyojengwa kwa nguvu za Wananchi Nzega.

**56. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali italitengeneza na kulitangaza Daraja la Mungu la kihistoria lililopo Wilaya ya Rungwe ambalo lipo katika hali ya kutotunzwa.

**57. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya uhaba wa Walimu katika Halmashauri ya Mji Nanyamba.

**58. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu ya maji mashuleni ili kuepuka milipuko ya magonjwa.

**WIZARA YA NISHATI:**

**59. MHESHIMIWA KHAMIS YUSSUF MUSSA (KWAHANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itainufaisha Zanzibar katika matumizi ya Nishati ya Gesi kutumika kwenye magari.

**WIZARA YA MAJI:**

**60. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini mpango wa kuhakikisha Vijiji vya Mkalama vilivyopo umbali wa Km 20 litakapopita Bomba la Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria vinapata maji.

**61. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Ichenjezya, Hasamba, Nwansana, Vwawa hadi Ilolo utakamilika na kuanza kutoa maji ya uhakika.

**WIZARA YA AFYA:**

**62. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itatoa majibu ya tafiti zilizofanywa Kanda ya Ziwa kubaini visababishi vya Kansa iliyokithiri.

**63. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwasaidia matibabu ya ngozi Watu wenye Ualbino kutokana na Ugonjwa wa Saratani ya Ngozi kuongezeka.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**64. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itatafsiri upya *Liquor and Intoxication Act, 1968* ili kutoa fursa kwa Wakulima wa Korosho kupata kipato kwenye Gongo ya Mabibo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**65. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini TANAPA watatumia vizuri fursa za Misitu waliyonayo kunufaika na Biashara ya *Carbon* kama nchi nyingine zinavyonufaika.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**66. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gari la Zimamoto Wilaya ya Nyang'hwale.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**67. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha Watanzania kununua bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini.

**WIZARA YA KILIMO:**

**68. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza kununua Mahindi ya Wananchi wa Jimbo la Ngara kupitia NFRA.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **14 APRILI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |